**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,**
Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na viumbe vyote, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kuweza kukutana katika Baraza hili la Kumi, kwenye Mkutano huu wa Kumi na Moja kwa lengo la kuendesha shughuli za kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako wote kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, kwa umahiri na weledi wa hali ya juu. Nikiamini kwamba uadilifu wenu huo wa hali ya juu ndio chachu ya kuimarika kwa Demokrasia katika muhimili huu muhimu wa dola katika nchi yetu hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Pia, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kuniamini na kunipa mashirikiano makubwa ambayo yameniwezesha kufanikisha kazi zangu kwa wepesi, kwa hakika ni wajumbe mahiri wenye uweledi, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima na taadhima, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Abass Wadi - Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Haji Omar Kheri - Mjumbe
6. Mhe. Zawadi Amur Nassor - Mjumbe
7. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
8. Ndg. Mussa Issa Mussa - Katibu
9. Ndg. Azmina Hamad Khamis - Msaidizi

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kumaliza utangulizi huo, naomba sasa nichukue nafasi hii adhimu kutekeleza jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako tukufu nalo ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya kila mwaka. Hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha **2023/2024.**

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mwaka huu wa fedha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Tatu (3) ambapo utekelezaji wake unasimamiwa na Programu Ndogo Tano (5).

## PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII

**Mheshimiwa Spika,**
Programu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Hifadhi ya Jamii **(SH040101)** kwa lengo la kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
Wakati Kamati ilipokuwa ikipitia Bajeti ya Wizara hii ilihoji juu ya suala

zima la uendeshaji wa Pencheni Jamii pamoja na upatikanaji wa Vitambulisho vya Wazee wanaopokea Pencheni hiyo. Kamati ilijibiwa kuwa huduma hii haitokuwa inasimamiwa tena na Wizara hii na kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 huduma hii itakuwa inatolewa chini ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inashauri Serikali licha ya huduma hiyo kuhamishiwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, ni vyema kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwani wao ndio wenye jukumu la kufuatilia ustawi wa jamii katika Taifa hili kwa mujibu wa Sheria.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika,**
Lengo kuu la kuanzishwa kwa Programu Kuu hii ni kusimamia masuala ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti pamoja na Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inashangazwa kwa kuona Wizara hii inakodi eneo katika jengo la Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*) liliopo Kinazini, eneo ambalo haliwatoshelezi kwa ajili ya utendaji wa kazi zao za kila siku, hali inayowapelekea Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri pamoja na baadhi ya watendaji kufanya kazi katika maeneo mbali na Makao Makuu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na kadhia hiyo, Kamati inaiomba Serikali kuirudisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika jengo lake la Mwanakwerekwe, jengo ambalo lilijengwa kwa fedha za Wafadhili pamoja na Serikali ili Wizara iweze kufuatilia vyema masuala ya ustawi wa jamii.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA

**Mheshimiwa Spika,**

Dhumuni kuu la kuwepo kwa Programu Kuu hii ni kutoa huduma ya Mapambano dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia pamoja na kutoa Huduma ya Maendeleo ya Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**
Vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto, vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku licha ya kuwepo kwa Sheria kali pamoja na kuanzishwa kwa Mahakama Maalum ya kushughulikia Masuala ya Kesi za Udhalilishaji. Kamati imebaini kusuasua kwa kesi hizo na kupelekea wananchi kuvunjika moyo sana.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Mahakama kuzisimamia, kuzisikiliza na kutoa maamuzi ya haraka kuhusiana na kesi hizo, ili kuwapa moyo wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji na kuona haki inatendeka kwani "Haki iliyocheleweshwa ni haki iliyokosekana".

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena, wewe binafsi, Mheshimwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni kwa niaba ya Kamati yangu, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa.

Sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na baadaye wawapitishie Bajeti ya Wizara hii ambapo jumla ya **Shilingi 9,887,311,00/= (Bilioni Tisa, Milioni Mia Nane na Thamanini na Saba, Laki Tatu na Elfu Kumi na Moja)** kwa ajili ya matumizi na jumla ya **Shilingi 20,000,000/= (Milioni Ishirini)** kwa ajili ya mapato na hatimae waikubali na waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa fedha unaokuja 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,**
Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, naiunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

…………………………….

**Mhe. Mohamed Ahmada Salum,**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**